# LEARNING BY EAR

## Lent luxury – The risks of raising credit

## EPISODE ONE: THE BIKE

**AUTHOR: James Muhando**

**EDITORS: Adrian Kriesch, Friederike Müller**

**PROOFREADERS: Tony Dunham, Pendo Paul**

**TRANSLATOR: Eric Ponda**

**<u>LIST OF CHARACTERS BY SCENE</u>**

**<u>SCENE ONE: JD'S SPANKING NEW BIKE</u>**

- **NARRATOR (M 30)**
- **JD (M 15)**
- **JENNY (F 15)**
- **GIDDY (M 15)**
- **1 STUDENT (F 14 - 17)**
- **TOBBY (M 17)**

**<u>SCENE TWO: SULKY GIDDY</u>**

- **NARRATOR (M 30)**
- **GIDDY (M 15)**

- **LUCIA (F 13)**
- **ZILPAH(F 35)**

**SCENE THREE: AT SCHOOL**

- **JENNY(F 15)**
- **GIDDY(M 15)**
- **NARRATOR(M 30)**
  - **YOUNG CROWD (min. 6, c. 15 years old, mixed gender)**

**SCENE FOUR: ON THE ROAD.**

- **JD (M 15)**
- **TOBBY (M 17)**
- **TRUCK DRIVER (M 40)**

**INTRO:**

**1. SFX: OFFICE ATMO**

**2. Narrator:**

Hujambo na karibu kwenye mfululizo wa vipindi vipya kabisa vya Learning by Ear , “Noa Bongo Jenga maisha yako” kwa jina Starehe za kuazima.- “Gharama ya mkopo”. Karibuni katika ofisi yangu. Jina langu ni Gideon Leboo. Na nafanya kazi katika benki hii ndogo kama Afisa anayehusika na utoaji mikopo na nitawaongoza katika mfululizo wa vipindi hivi. Na nisingependa kuwachokesha na hadhithi ndefu kuhusu kazi yangu ninayofanya. Lakini labda mtashangaa kusikia kwamba

nilikuwa kijana mtukutu sana, kama nyinyi tu! Nilizaliwa miaka 30 iliyopita katika kijiji cha Kwanza sio mbali sana kutoka hapa . Na nilipokuwa kuwa shuleni ndoto yangu nilitaka sana kuwa wakili pindi ninapokamilisha masomo yangu. Pengine naenda haraka haraka sana, tuanzie mwanzo kabisa nilipokuwa nikifahamika kama Giddy hadi nilipofika sasa ambapo nafahamika kama Gideon Leboo afisa wa mikopo katika benkii. Ilikuwa mwezi Januari miaka 15 iliyopita, likizo ilikuwa ndio mwanzo imemalizika na shule zinaenda kufunguliwa. Nilikuwa na hamu sana ya kukutana tena na rafiki zangu Jenny na JD! na kwa hakika walikuwa na mengi ya kusimulia baada ya likizo hiyo ndefu!

## SCENE ONE: AT SCHOOL

**3. SFX:** **SCHOOL AMBIENCE, STUDENTS MAKING NOISE, BICYCLES BELL RINGING.**

**4. JENNY**: **(Shouting)** Giddy, Giddy, njoo hapa!

**5. GIDDY:** **(From far)** Jenny, nisubiri naja!

6. **JENNY:** Hee, na umekuwa mkubwa!umekula nini wakati wa likizo. Hebu njoo hapa na sura yako hiyo iliyo nona nikukumbatie! **(They hug as they laugh).**

7. **GIDDY:** **(Laughing)** Hebu mtazame anayezungumza, umenenepa hata siwezi kukumbatia.

.

8. **JENNY:** Ni kweli!

9. **GIDDY:** Likizo ilikuwaje

10. **JENNY:** Likizo imekuwa nzuri.

Ama kwa hakika Giddy umekuwa mkubwa, na kisha ni miezi miwili tu! Kwani umekuwa ukila nini?

11. **GIDDY:** **(Jokingly)** Ahhhh! Nyamaza, kwanza sitaki kuzungumza na wewe.

12. **JENNY:** Aha? Kwa nini?

13. **GIDDY:** **(Mimics her)** Nyenye! Nyenye! Wewe ni rafiki wa aina gani unasafiri kutoka mjini bila ya taarifa?

14. **JENNY:** Wewe ni mwanamume unayeweza kustahamili. Habari ya JD?

15. **SFX:** **BICYCLE BELL RINGING FROM FAR, BICYCLE APPROACHING**

**16. GIDDY:** Muulize mwenyewe. Ndio huyo anafika. Kisha na Beskeli mpya! Hamjambo? Mbona hakuna mtu anataka kunizungumzia siku hizi!

**17. JENNY:** **(Jokingly)** Pengine ni kwa sababu ya udaku wako ! **(Shouts)** Wewe kijana! Ondoka hapa

**18. SFX:** **BRAKES OF BICYCLE**

**19. JD:** **(As he dismounts the bike)** JD! Jina langu ni JD. Kwani mara ngapi nitakwambia isiniite Junior?

**20. JENNY:** Sawa, utakavyo !

**21. GIDDY:** **(Sarcastically)** Huh! Siku hizi JD amenunua baiskeli mpya.

**22. JENNY:** Na si baiskeli tu, Sport bike!

**23. JD:** Sikizeni si baiskeli hizi za kawaida, yake ni ya kisasa, aina ya BMX sports bike na inagia sita.

**24. THEY ALL LAUGH.**

**25. STUDENT:** **(From far)** Wow! Hebu itazame!

**26. TOBBY:** **(From far)** Habari JD! Baiskeli yako ni nzuri sana. Naweza kujaribu?

**27. NARRATOR:**

Siku hiyo, rafiki yangu JD alipata marafiki wengi sana wote wakitaka kujaribu kuendesha baiskeli yake mpya. Hata alitupuuza mimi  na Jenny kwani alitaka kutangamana na marafiki wanaotajika shuleni. Lakini je urafiki huo ungedumu kwa muda gani? Tulitaka sana kujaribu kuendesha baiskeli yake. Rafiki yangu JD alipata marafiki wengi waliotaka kujaribu baiskeli yake. Isitoshe alitupuuza mimi na Jenny kwa sababu alitaka kutangamana na marafiriki wanaotajika shuleni. Lakini urafiki huo utadumu kwa muda gani? Hayo ni baadaye, lakini jioni hiyo nyumbani kwangu....

## SCENE TWO: AT GIDDY’S

| | | |
|---|---|---|
| **28.** | **SFX:** | **INSIDE HOME, RADIO** |
| **29.** | **SFX:** | **DOOR OPENING.** |
| **30.** | **ZILPAH:** | **(Humming a tune to herself)** |
| **31.** | **SFX:** | **KICK AGAINST BAG** |
| **32.** | **ZILPAH:** | **(Stumbling over bag)** Ni nini tena..? Mvulana huyu! Mara ngapi nitakwambia uweke vizuri chumbani mkoba wako wa shule kila unapotoka shule! **(Shouts)** Giddy! Giddy! Njoo hapa upesi! |
| **33.** | **SFX:** | **FOOTSTEPS** |
| **34.** | **SFX:** | **KNOCK ON THE DOOR.** |

**35. ZILPAH:** **(Still shouting)** Giddy najua uko ndani. Usinikasirishe nakaja kukuvuta masikio hapo. Toka hapa nje upesi!

**36. SFX:** **DOOR OPEN.**

**37. GIDDY:** **(Sulking)** Nimefika mama!

**38. ZILPAH:** **(Mimics him)** Mama yangu! Hii ni nini?

**39. GIDDY:** Ni mkoba wa shule.

**40. ZILPAH:** Wa nani?

**41. GIDDY:** Wangu!

**42. ZILPAH:** Na unafanya nini hapa sebuleni kisha sakafuni? Nimesema nini kuhusu tabia hii ya kurusha mkoba wako wa shule kwenye sakafu hapa sebuleni?

**43. GIDDY:** Kwamba nisiwe nikirusha mkoba wangu wa shule ovyo ovyo….

**44. ZILPAH:** **(Cuts in)** Na badala yake.

**45. GIDDY:** Niuweke vizuri chumbani

**46. ZILPAH:** Na … hapa unafanya nini?

**47. GIDDY:** Lakini mama, nimechoka! Nimelazimika kutembea kutoka shuleni. Watoto wengine wote wanaendesha baiskeli!

**48. SFX:** **FOOTSTEPS APPROACH.**

**49. LUCIA:** **(In a nosy way)** Mimi sina Baiskeli na hujanisikia nikilalamika hata siku moja!

**50. GIDDY:** Funga domo lako Lucia, sitaki kimbelembele chako!

**51. ZILPAH:** Dadako anakwambie ukweli kwani lazima baiskeli ndio uweze kuwa muajibikaji? Hebu uondoe huu mkoba wako haraka hapa!

**52. LUCIA:** Najua kwanini amenuna mama, ni kwa sababu rafiki yake JD ana baiskeli mpya.

**53. GIDDY:** Kwanini usifuate shughuli zako mpumbavu wewe! Mimi sizungumzi na wewe!

**54. ZILPAH:** Aha! Kwa hiyo ndiyo sababu, huh? Hebu nisikilizeni nyinyi wawili, tena mnisikilize kwa makini sana, msijaribu hata siku moja kujifananisha na wengine maishani. Sawa? Hamjui JD anatoka familia yenye uwezo kiasi gani.

**55. GIDDY:** Lakini mama yao ni maskini tu kama sisi!

**56. ZILPAH:** Sawa hata kama ni maskini kama sisi, lakini unafahamu kwamba asilimia 99 ya matatizo yanayotukumba yanatokana na kasumba hii ya kujilinganisha na wengine?

**57. NARRATOR:**

Yote niliyojaribu kusema, mama hakutaki kusikia la muadhini au mteka maji. Nilichohitaji zaidi ni baiskeli, na nilihitaji zaidi ya alivyofikiria.

Nilienda kulala nikiwa nimenuna sana! Baadaye nilishtuliwa kutoka usingizingi na sauti iliyofanana na ya mamangu na kengele ya baiskeli.

**58. SFX:** **BICYCLE BELL**

**59. ZILPAH:** Amka wewe mtoto mvivu! Amka haraka! Utachelewa kwenda shule!

**60. GIDDY:** **(Sleepily)** Niache.

**61. ZILPAH:** Amka nimekununulia baiskeli mpya.

**62. GIDDY:** **(Suddenly all happy)** Baiskeli! Oh! Asante sana! Asante sana Mama! Baiskeli mpya mama!

**63. LUCIA:** **(Laughs)**

**64. NARRATOR:**

Tatizo ni kwamba ilikuwa ndoto tu. Kumbe nilikuwa nimeamshwa na kengele ya saa na kumuona dadangu Lucia pia akijaribu kuniamsha huku akinichekea.

**65. SFX:** **ALARM BELL**

**66. GIDDY:** **(Wakes up from dream muttering)** Baiskeli, Baiskeli mpya sasa iko wapi?

**67. LUCIA :** **(Laughing heartily)** Utachelewa kwenda shuleni. Unazungumzia baiskeli gani wewe mtoto mvivu?

**(Shouts)** Mama! Mama ! Giddy anaota kuhusu baikseli. mpya!

**68. GIDDY:** **(Angry)** Toka chumbani mwangu! Tena haraka upesi! Kwani huwezi kusoma, maandishi mlangoni yanasema “ Usiingine”!

**69. SFX:** **FAST LEAVING FOOTSTEPS**

**70. LUCIA:** **(Sings in mockery as she runs)** Giddy anaota! Giddy anaota!

## SCENE THREE: AT SCHOOL

**71. SFX:** **AFTER SCHOOL AMBIENCE. CHILDREN GOING HOME. BELLS RINGING. SHOUTING ETC.**

**72. JENNY:** **(Shouts jokingly)** Giddy sura mbaya.

**73. GIDDY:** **(Laughs)** Jenny! Nifanyaje ndio ukome kuniita jina hilo?

**74. JENNY:** Hakuna. Kila siku uje shuleni ukikimbia!

**75. GIDDY:** Na unapozungumzia kukimbia. Hebu twende tukamtafute JD haraka. Alituahidi kutupatia baiskeli yake tuendeshe kidogo!

**76. JENNY:** Hata hujamaliza kusema , ndio huyoo....

**77. GIDDY:** Na, yule ni Tobby wanayetembea naye?

**78. JENNY:** Siamini macho yangu! Siku zote Tobby ametudhulumu na kutuita nyang’au.

**79. GIDDY:** Usijali. Sasa anajaribu kutukwepa. Muone hataki hata kutuangalia.

**80. JENNY:** JD! JD!

**81. GIDDY:** Muache Jenny! Huoni anajaribu kututoroka?

**82. NARRATOR:**

Hivyo ndivyo, JD alivyoweza kuwatoroka rafiki zake wa jadi na kushikana na Tobby, mvulana mwenye maringo shuleni. Kwa muda mrefu Tobby amekuwa akiwadharau na kuwatendea dhuluma za kila aina marafiki hawa watatu. Lakini, baada ya muda si mrefu, JD anafahamu kwamba Tobby hawezi kuendesha baiskeli.

**<u>SCENE FOUR: ON THE ROAD.</u>**

**83. SFX:** **LIGHT UPCOUNTRY TRAFFIC, SCHOOL NOISE IN BACKGROUND**

**84. TOBBY:** Shikilia baiskeli nipande.

**85. JD:** Unamaanisha nini? Nilidhani wewe ni mjuzi wa kuendesha baiskeli!

**86. TOBBY:** Najua kuendesha, nataka tu unishikilie nipande.

**87. JD :** Kama kweli unajua kuendesha hungeniomba nikushikilie upande!

**88. TOBBY:** **(Aggressively)** Aaah! Sasa utanisaidia kushikilia baiskeli ama la?

**89. JD:** Sawa lakini uwe muangalifu.

**90. SFX** **Bike riding sounds**

**91. TOBBY:** **(as he rides off starts to laugh, satisfied)** Unajua mimi ni dume! Wewe sasa nitaisimamisha vipi?

**92. SFX:** **TRUCK APPROACHES**

**93. JD:** **(Shouts alarmed)** Kuwa muangalifu kuna lori. Tobby ruka! Ruka!

**94. SFX:** **THUD AS SOMEONE JUMPS. SCREECHING TIRES AS TRUCK CRUSHES BICYCLE.**

**95. TRUCK DRIVER:** **(Shouts)** Msicheze barabarani nyinyi vijana wapumbavu. Kuna mtu ameumia?

**96. JD:** **(Shouts back)** Tuko salama, lakini baiskeli yangu imebonyea.

**97. TRUCK DRIVER:** Hilo ni funzo kwenu! Sitalipa gharama ya kuharibika kwa baiskeli!

**98. SFX:** **TRUCK DRIVES OFF**

**99. TOBBY:** **(Panting, scared)** Mungu wangu, nusra tu! Nimeshikwa na uoga!

**100. JD:** Baiskeili yangu. Hebu tazama ulivyoifanya baiskeli yangu!

**101. TOBBY:** **(Not remorseful)** Samahani sana .

**102. JD**: Samahani, yaani hilo ndilo unaloweza kusema. Nimenunua baiskeli hii kwa mkopo! na hata sijamalizia kuilipia.

**103. TOBBY:** Nimesema samahani sana.

**104. JD:** Hebu tazama imeharibika kabisa.

**<u>OUTRO</u>:**

**102. NARRATOR:**

Baiskeli ya JD imeharibika kabisa kiasi cha kutorekebishika. Na Tobby hata hajali kwa yote yaliyotokea. Muda wote huo sisi marafiki na hata wazazi wake tulidhani JD alinunua Baiskeli hiyo pesa taslimu lakini kumbe sivyo kabisa, tumekuja kufahamu baadaye kwamba aliichukua kwa malipo ya pole pole. Na hata kabla ya kumaliza kuilipia, baiskeli hiyo imeharibika kabisa. Je nini kitakachotokea baadaye?

**103. SFX:** **PAPERS RUSTLE.**

**104. NARRATOR:**

Hadi hapo tunafika mwisho wa makala ya leo ya Noa Bongo jenga maisha yako. Ungana nasi kwa makala nyingine kwenye kwenye mfululizo wa vipindi kumi katika mchezo “Starehe ya Kuazima”- “Tatizo la kugharamia mkopo”. Iwapo ungependa kusikiliza tena makala haya tembelea mtandao wetu wa dw.de /lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.